THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

021

# KISWAHILI

MUDA: Saa 3 13 Januari 1999 MCHANA

**Maagizo kwa Watahiniwa**

1. Jibu maswali MANANE (8) tu, maswali MANNE (4) kutoka sehemu A, na maswali YOTE Sehemu B.
2. Zingatia maagizo ya kila SEHEMU na ya kila swali.
3. Andika namba YAKO ya mtihani katika kila ukurasa unaotumia wa kijitabu chako cha majibu.

9021

Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU A: FASIHI

### Kifungu (i): Fasihi Simulizi

1. Hadithi ni utanzu wenye dhima kubwa katika burudani na elimu katika fasihi simulizi. Unaitofautishaje dhima hii na ile ya fasihi andishi? (alama 15)

AU

2. Maendeleo ya kisasa ya kijamii na ya kiuchumi ni matishio kwa usitawi wa fasihi simulizi: hasara inoyotukabili kutokana na matishio hayo ni makubwa. Jadili ukitoa mifano. (alama 15)

### FASIHI ANDISHI

### Kifungu (ii) Ushairi

| VITABU | | |
|---|---|---|
| Malenga Wapya | TAKILUKI | (D.U.P) |
| Diwani ya Mloka | C. MLOKA | (B.P.) |
| Diwani ya Ustadh | A. Andanenga | (B.P.) |

3. Mshairi mzuri si mkwasi wa lugha tu, bali pia mtumiaji wa lugha kisanaa na kwa uangalifu azungumziapo jambo. Chagua vitabu viwili kati ya hivyo vilivyotajwa hapo juu, ili uthibitishe kauli hii. (alama 15)

AU

4. Mshairi si shabiki wa mambo, bali ni msanii na mchambuzi wa masuala ya kijamii na maisha. Jadili kauli hiyo ukitumia vitabu viwili kati ya hivyo vilivyotajwa hapo juu. (alama 15)

### Kifungu (iii): Riwaya/ Hadithi

| VITABU | | |
|---|---|---|
| Kusadikika | S. Robert | (Nelson) |
| Hiba ya Wivu | Z. Mwanga | (R.P.) |
| Zawadi ya Ushindi | B. Mtobwa | (T.P.H.) |

5. Wahusika katika riwaya hutusaidia kutuonesha maisha kuliko tuwezavyo kuyaona katika mazingira ya maisha halisi tunamoishi. Jadili kauli hii kwa kutumia vitabu viwili kati ya hivyo vilivyotajwa hapo juu. (alama 15)

AU

6. Ujasiri na uadilifu ni misingi isiyotenganishwa katika ujenzi wa jamii yenye usitawi. Unakubali? Thibitisha jibu lako kwa kutumia vitabu viwili kati ya hivyo vilivyotajwa hapo juu. (alama 15)

### Kifungu (iv): Tamthiliya

| VITABU | | |
|---|---|---|
| Ngoswe - Penzi Kitovu cha Uzembe | E. Semzaba | (ESC) |
| Mfalme Juha | F. Topan | (DUP) |
| Hawala ya Fedha | A. Lihamba | (T.P.H) |

7. Aghalabu watu hutenda makosa kwa kutaka kutenda makosa hayo au kwa ujinga wa kutojua kama watendalo ni kosa. Jadili kauli hii kwa kutumia vitabu viwili kati ya hivyo hapo juu. (alama 15)

AU

8. Watanzania wa leo wangefaidika sana na Tamthiliya kama wangekuwa na utamaduni wa tamthiliya. Thibitisha kauli hii kwa kutumia vitabu viwili kati ya hivyo vilivoytajwa hapo juu. (alama 15)



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner

## SEHEMU B - LUGHA

9. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali:

Ushairi hauwezi kutenganisha na jamii kwani ushairi umekuwa ukikua na kuendelea kadiri jamii inavyokua na kuendelea. Mabadiliko yoyote yaliyotokea yawe ya muundo, fani na maudhui - yalitokea vivi hivi, bila kulazimishwa wala kukongamaniwa. Mabadiliko haya kwa kuwa yalitokana na umma wa watu na manju wenyewe yalipokewa bila upinzani wowote; yalikuwa mabadiliko yenye nia nzuri ya maendeleo.

Kwa kuwa ushairi umetokana na jamii ya mwanadamu mwenyewe, utaona kuwa umsheheneza ukwasi mkubwa wa lugha ambayo imekuwa ikitumika katika hatua zote za kisasa, kiuchumi na kiutamaduni katika historia ambayo mwanadamu amepitia. Kwa mfano, kuna msamiati uliotumika tangu enzi za kuishi mapangoni, enzi za wageni, ukoloni, harakati za kupambana na ukoloni hadi kupatikana kwa uhuru, na maendeleo yake. Kwa kuwa hivi sasa mawasiliano baina ya mwanadamu na mwanadamu, au taifa na taifa, yamekuwa bora zaidi, ushairi haukujifunga kizuizi, bali umenesa na kuchukua msamiati wenye dhana na fikra za kimataifa. Na maendeleo yote hayo hayakukongamaniwa.

Iwapo twakubaliana na hayo, basi chimbuko la mshairi wa Kiswahili ni nini? Yapo maoni mengi kuhusu swala hili. John Ramadhani anasema kuwa chanzo cha ushairi ni "hisia au mchomo unaosababishwa na mazingira", ambayo anazidi kutueleza kuwa hali ya kishairi inahusiana kidogo na hali ya kindoto, au tabia ya kuona yasiyoonekana, na kuwania yasiyowezekana. Fikra za John Ramadhani zina walakini kidogo, kwani ushairi hauhusiani hata kidogo na ndoto; wala mshairi hana uwezo wa kuona yasiyoonekana. Sababu ya kuzikanusha fikra hizi ni kwamba mshairi hutungia mazingira yake na katika kutunga kwake huweza kuzizamia kwa undani taasisi za jamii yake akazihakiki. Katika kufanya hivyo huzikosoa, huzielekeza, huzishauri na pengine huzitanakisha. Kwa kuwa mshairi huisoma na kuielewa jamii yake vizuri, mambo atahadharishayo kama hayakufanyiwa marekebisho mapema baadaye huja yakazua watu kufikiri kwamba mshairi ni mwota ndoto za kweli, kumbe sivyo; ni weledi wake tu, kwani shairi atungapo huunganisha pamoja sanaa, fani na maudhui na lugha teule. Na hivi ndivyo vitu vinavyofanya tungo zake zidumu.

MASWALI:

(a) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari kama yalivyotumiwa katika habari uliyosoma.

(b) Kwa mujibu wa habari hii, mabadiliko katika sanaa na maudhui ya mshairi yametokana na nini?

(c) Teknolojia ya mawasiliano duniani yamechangia nini katika mshairi wa Kiswahili?

(d) Taja mawazo makuu mawili ambayo John Ramadhani anaona ndicho chanzo cha ushairi wa Kiswahili.

(e) (i) Baina ya mawazo haya mawili juu ya chanzo cha ushairi wa Kiswahili, mwandishi haafikiani na lipi?
    (ii) Kwa sababu ipi?

(f) Kwa maneno yasiyozidi sitini (60), fupisha aya ya mwisho ya kifungu hiki cha habari.

10. Andika insha isiyopungua maneno 250 juu ya mada moja kati ya mada zifuatazo:
   (a) Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe
   (b) Jamii isiyo na maadili ni sawa no kundi la wanyama pori
   (c) Maisha yangu katika shule yangu ya sekondari
   (d) Umuhimu wa kujisomea
   (e) Athari za mafuriko ya mwaka jana

(alama 10)

11. (a) Eleza hatua tano za uchanganuzi wa sentensi
   (b) Tumia hatua hizo tano kuchanganua sentensi kwa njia ya matawi
   "Ng'ombe anakula majani makavu usiku na mchana"

(alama 10)

12. Sahihisha sentensi sifuatazo. Kwa sentensi zisizo na makosa, andika neno "sahihi".
   (a) Waziri wa Sheria aliwakilisha muswada Bungeni
   (b) Sote twapashwa kufuata sheria, la sivyo, tutaadhibiwa
   (c) Nilifika nyumbani kwake, lakini sijamkuta
   (d) Sijakutana naye hata siku moja
   (e) Ukishafika uniandikiege barua dada!

(alama 10)



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

Scanned with CamScanner